

UTANGULIZI

Utawala bora ni nguzo mojawapo muhimu katika kutekeleza MKUKUTA (Mkakati wa Kukusa Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania), ambayo inahimiza uwazi na uwajibikaji katika ngazi zote za uongozi. Kwa jamii iliyopokea vizuri mpango huu wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu, ni vizuri viongozi wake wakawa wazi na wawajibikaji katika jamii au kamati husika.

UTAWALA BORA

Utawala bora ni mfumo ambao jamii inatakiwa kufuata ili kuweza kuwa na maendeleo endelevu yenye uwazi, ukweli na uwajibikaji. Lengo kuu la utawala bora ni kukuza maendeleo na kupunguza umasikini na mambo muhimu katika utawala bora ni uongozi bora, mipango na utekelezaji wake.

UONGOZI BORA

Ni uwezo au njia ya kuweza kuwashawishi watu ili waweze kufanya kitu au kufikia lengo fulani la kikundi kwa ridhaa yao wenyewe. Ili uongozi uwe bora ni lazima kuwe na kiongozi anayeongoza kundi fulani la watu au jamii husika.

KIONGOZI

Huyu ni mtu mwenye kuweza kuwashawishi wengine kufanya kitu au jambo fulani kwa uwezo wao wote ili kufikia malengo yaliyopangwa. Miongoni mwa sifa za kiongozi ni kama zifuatazo:-

- Mwajibikaji
- Mbunifu
- Mwenye upeo wa kuelewa mambo
- Mwenye uhusiano mzuri na watu
- Mwenye msimamo thabiti
- Mwenye uwezo wa kuandaa mipango na kusimamia utekelezaji wake
- Mwenye uwezo wa kutoa ushauri wenye busara
- Mwenye kujiamini
- Mwenye kukubali ushauri bila ubishi *na*
- Mwenye ari (mwenye kuipenda kazi yake)

MIPANGO

Ili kuweza kutekeleza mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ni vizuri kwa kamati ya maliasili ya kijiji kujiwekea mpango kazi au mwongozo maalumu wa kufuata. Zipo aina mbili za mipango, ambayo ni mipango ya muda mfupi na mipango ya muda mrefu. Mipango ya muda mfupi, hii ni mipango

ambayo inalenga shughuli za kila siku, wiki, mwezi hadi mwaka mfano ratiba za vikao au mikutano, shughuli zinazofanywa na kamati ya maliasili kama vile doria, kubabua moto, kufyekea mipaka na kufanya tathmini shirikishi ya mazao ya misitu. Mipango ya muda mrefu ni ile yenye malengo marefu ambapo shughuli zake zinakuwa kuanzia mwaka mmoja, miwili, mitatu na kuendelea.

UTEKELEZAJI

Mipango yote iliyo pangwa, mfano kuitisha vikao, kufanya doria ni lazima itekelezwe ili kuweza kuwa na utawala bora au uongozi bora. Utekelezaji wa mipango iliyopangwa na kamati ya maliasili imegawanyika katika sehemu kuu mbili nazo ni ufuatiliaji na utoaji wa taarifa. Ufuatiliaji unaweza kuwa ni wa kufuatilia mipango iliyowekwa kama haijaenda vizuri ili kutatua tatizo lililopo au kufuatilia utendaji wa kazi kama unaenda vizuri au hapana.

Katika kutekeleza mpango wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu, utoaji wa taarifa ni muhimu katika ngazi zote za kijiji kuanzia ndani ya kamati yenyewe ya maliasili ya kijiji, serikali ya kijiji na mkutano mkuu wa kijiji. Utoaji huu wa taarifa katika ngazi zote za kijiji utasaidia ukweli, uwazi na uwajibikaji ndani ya kamati ya maliasili na hivyo kuzuia

rushwa na jamii itaamini watendaji wake ndani ya kamati ya maliasili.

Baadhi ya taarifa muhimu ambazo zinapaswa kila mtu katika ngazi ya kijiji afahamu ni kama vile, taarifa kuhusu kikao au mkutano, taarifa za fedha (mapato na matumizi). Taarifa hizi zitasaidia wanajamii kujua nini kinaendelea katika kamati ya maliasili au uongozi wa serikali ya kijiji na hivyo kuuamini uongozi wa kijiji au kamati ya mali asili.

UTUNZAJI WA KUMBUKUMBU

Utunzaji wa kumbukumbu ni muhimu katika maisha yetu ya kila siku. Kumbukumbu husaidia kukumbuka kazi uliyokwisha fanya na ambayo unatarajia kufanya. Hivyo basi ni muhimu kwa kamati ya maliasili ya kijiji kuweka kumbukumbu katika shughuli wanazofanya juu ya Usimamizi Shirikishi wa Misitu. Kwa mfano kumbukumbu za mikutano au vikao ndani ya kamati, kumbukumbu za pesa (mapato na matumizi) au kumbukumbu ya adhabu (fidia) kwa mharifu wa rasilimali za misitu. Kumbukumbu kama za pesa (mapato na matumizi) au fidia ni vizuri kwa Mweka hazina wa kamati ya maliasili kuwa na

stakabadhi ambayo itaidhinisha mapato au matumizi au fidia iliyolipwa na mharifu.

UTUNZAJI WA PESA

Pesa zote zinazohusiana na kamati ya maliasili zitahifadhiwa benki. Kamati maliasili inashauriwa kufungua akaunti maalumu ya kutunza pesa zinazotokana na rasilimali za misitu. Kiasi kidogo cha pesa kinaweza kubaki kwa mtunza hazina kwa ajili ya dharura na matumizi madogo madogo ya kamati.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Mradi wa Kuhifadhi Mpingo au Idara ya Maliasili Wilaya ya Kilwa, S.L.P. 49, Kilwa Masoko.



Kijarida hiki kimeandaliwa na Mradi wa Kuhifadhi Mpingo (MCP) kwa msaada wa Darwin Initiative (Uingereza).

Utawala Bora na



Usimamizi Shirikishi wa Misitu